| | |
|---|---|
| **Kichwa cha mradi** | Mradi wa Kasigau corridor REDD+Project Phase II Community Ranches |
| **Kitambulisho cha mradi** | 612 |
| **Toleo** | 1.7 |
| **Kitambulisho cha Ripoti** | 1 |
| **Tarehe ya suala** | 31-Julai-2018 |
| **Eneo la Mradi** | Kenya, Kaunti ya Taita Taveta, Mkoa wa Pwani |
| **Wasaidizi wa Mradi** | Wildlife Works Carbon LLC.: Rais – Mike Korchinsky<br>Tel: +1-415-332-8081<br>Fax: +1-415-332-8057<br>Email: jeremy@wildlifeworks.com |
| **Mtaarishi** | Jeremy T. Freund and Simon C. Bird |
| **Bodi ya Uthibitisho** | SCS Global Services<br>Francis Eaton<br>2000 Powell Street, Ste. 600, Emeryville, CA 94608 USA<br>+1-510-452-8000<br>FEaton@scsglobalservices.com |
| **Uhasibu wa GHG / kipindi cha mradi** | 01 Januari 2010 – 31 Disemba 2039; 30-mda kamili wa mwaka |
| **Muda uliotumika kutathmini ripoti hii** | 01 Januari 2015 – 31 Disemba 2017 |
| **Historia ya hali ya CCB** | Uthibitisho wa CCB: 27 Aprili 2011<br>Uthibitisho wa CCB M1: 25 Mei 2011<br>Uthibitisho wa CCB M2: 5 Decemba 2012<br>Uthibitisho wa CCB M3: 23 Mai 2013<br>Uthibitisho wa CCB M4: 01 Novemba 2016 |
| **Kiwango cha toleo la CCB Kilicho tumika kwa uthibitisho** | Mradi huu unathibitishwa katika toleo la pili la kiwango cha CCB |
| **Vigezo vya juu** | Mradi wa Kasigau Corridor REDD+ awamu ya kwanza umeafikia viwango vya juu kwa utoaji faida unaotokana na utunzi wa mazingira na pia kuweza Kuangazia uhifadhi wa bionuwai<br><br>**Manufaa yanayo patikana na kuzuia mabadiliko ya tabia nchi**<br><br>Kuna Ushahidi wa kutosha unaoonyesha kuwa kuna mabadiliko ya tabia nchi katika maeneo ya mradi. Tangu jadi jamii zinazoishi kwa eneo la mradi wamekua wakitegemea sana kilimo. Eneo la mradi ni baadhi moja wapo ya maeneo ambayo hayana rotuba ya kufanya kilimo nchini Kenya. Mvua imepungua kwa miaka Kadha iliyopita, hii imesababisha kudorora kwa upanzi katika mda unao stahili. Shida hii itaongezeka kutokana na mabadiliko ya hali ya anga kwa miaka kadhaa ijayo. Matokeo ya ukosefu wa mavuno yamesababisha wakulima kuendelea kufungua maeneo ya misitu kwa matarajio ya |

kupata mvua ya kutosha. Tusipo linda misitu kutakuwa na ongezeko wa uharibifu wa misitu kama hali za hewa zitazidi kudorora. Ukosefu wa mavuno unasababisha uwindaji haramu. Idadi ya Wanyama pori asili wanaweza kujikimu wakati wa ukame, lakini pia hutaabika iwapo kuna mvua chache na joto jingi. Hii inamaanisha kwamba wanyama hawa wako katika hatari ya kuwindwa.

**Katika kipindi hiki cha utekelezaji mradi umeweza kutimiza yafuatayo:**

- Kupunguza utegemeaji wa ardhi na mifugo kupitia njia mbadala za IGA, kuchochea ukulima wa mimea inayo stahimili ukame, kuboresha vifaa vya kuhifadhi na usimamizi wa mazao, kuvuna na uhifadhi wa maji, kupeana mafunzo ya hatari ya moto.
- Kuongeza msaada wa miundo ya taasisi za mitaa ikiwa ni pamoja na kanuni na sheria za utawala kusaidia kuendeleza mikakati inayofaa, kuongeza viwango vya kujifunza, kuchanganua shughli za Maisha na mradi wa kizazi cha mpato, kuhusisha wanawake kwa kiwango kikubwa katika mchakato wa uamuzi, kuongeza ushiriki wa jumla katika uamuzi wa ngazi za ndani.
- Kusaidia kudumisha mazingira yanayowiana na ya ndani kupitia ulinzi wa mazingira, kuhakikisha urejesho wa mazingira ili kuruhusu uhamiaji, shughuli stadi za urejesho kutumia mimea ya kiasili inayo stahimili ukame.

**Faida zinazotokana na kuifadhi bionuwai**

- KCRPII ina aina ya pundamilia wa grevi ambao wako hatarini kwenye orodha ya ICUN Red. Rukinga inaweza kuwa na asilimia 3% ya idadi ya pundamilia wa aina ya grevi ambao wanakisiwa kuwa 750 katika mwaka wa 2008.
- KCRPII ni eneo wanapo patikana mbwa mwitu wa afrika (Lycaon pictus). Mbwa hawa wameweza kunaswa na picha za camera zilizoko Rukinga ambao pia wako hatarini kulingana na orodha ya IUCN Red.
- KCRPII pia imeweza kuhifadhi aina kadhaa za tai wakiwemo tai wenye rangi nyeupe mgongoni (Gyps africanus) na wale wa uso wa lappet (Turgos trachellutus). Wamo katika hatari Kubwa ya kuisha.
- KCRPII ina idadi nzuri ya Wanyama walio na thamani ya hifadhi ya juu na wako kwa hatari Kubwa ya kuisha wakiwemo Duma (Acinonyx jubatus), Simba (Panthera leo) ndege aina ya sekretari, tai aina ya Martial na tembo wa Afrika (Loxodonta Africana).
- Eneo la mradi ni moja wapo ya KIkundi la Eastern Arc Mountain Global Hotspot kama inavyo fafanuliwa na shirika Conservation International. Ndani ya eneo la mradi pamoja na nje ya mradi kuna aina nyenginezo za Wanyama kama vile: Taita Apali (*Apalis fuscigularis*), na Taita Thrush (*Turdus helleri*).
- Katika kipindi cha ufatiaji wa mradi kazi za msingi zilizofanyika ni kuhakikisha tumezuia uharibifu wa misitu katika eneo la mradi. Hii

| | |
|---|---|
| | imeweza kuboresha bionuai jinsi ilivyokuwa na jinsi inavyotakiwa kuwa. Eneo la mradi pia linaumuhimu kwani ni eneo lililoko na bionuai ya kila aina na pia ni baadhi ya maeneo yanayo shikanisha sehemu ambazo ni muhimu kwa maswala ya utunzi wa mazingira. Mwisho, eneo la mradi ni eneo ambayo wanyama wa pori hutumia kutoka eneo limoja kwenda linguine na hii imepunguza mkwaruzano kati ya wanyama pori na binandamu.<br>• Baadhi ya kazi za msingi zilizofanywa ni kuhakikisha kuwa tuko na mabwawa za maji za kutosha na pia kuhakikisha zipo katika hali iliyo bora. Hizi bwawa zimeweza kuweka maji ambayo hutumiwa na wanyama pori kwani eneo la mradi ni baadhi ya maeneo ambayo yako kwenye kiangazi. |

### 1.1 Faida za kipekee za mradi

| Matokeo | Yaliyotimizwa mdaa wa ufuatiliaji | Sehemu ya kumbu kumbkumbuku k | Yaliyoyimizwa wakati wa mradi unaendelea. |
|---|---|---|---|
| 1) GLOW (Girls Leading our World)<br>Wasichana wanaoongoza ulimwengu wetu. | Ilifanyika kwa shule, yaliyofundishwa ni afya ya uzazi, usafi wa mazingira na mwil. Mafundisho haya yalifanyika kwa shule 15 na kila shule wanafunzi 30-50 waliweza kuhudhuria | 2.1.1 | Ilifanyika kwa mashule yaliyofundishwa ni afya ya uzazi, usafi wa mazingira na mwili.<br>Mafundisho haya yalifanyika kwa shule 15 na kila shule wanafuzi 30-50 waliweza kuhudhuri. |
| 2) Hadithi | Husaidia kwa ununuzi wa bidhaa za kiasili kutoka kwa vikundi 31, inayohusisha wanawake wasiopungua 800.Makadirio ya kiwango cha fedha yaliyoilipa vikundi hivi tokea mwaka wa 2015-2017 ni USD100000. | 2.1.1 | Husaidia kwa ununuzi wa bidhaa za kiasili kutoka kwa vikundi 31, inayohusisha wanawake wasiopungua 800.Makadirio ya kiwango cha fedha yaliyolipa vikundi hivi tokea mwaka wa 2015-2017 ni USD 100000. |
| 3) Utalii | Imeajiri kati ya wafanyikazi 4-10. | 2.1.1 | Imeajiri kati ya wafanyikazi 4-10. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Takriban wageni 500 kwa mwaka wanaokaa hoteli ya kivuli na imeleta faida ya USD3000 hadi 7000 | | Takriban wageni 500 kwa mwaka wanaokaa hoteli ya kivuli na imeleta faida ya USD3000 na 7000 |
| 4) Uzalishaji wa makaa zingira | Imeajiri wafanyikazi 8 wa kudumu. Kuanzisha mfumo wanaonatengeneza makaa zingira kwa njia ya kitaalamu. | 2.1.1 | Upelezi wa kupimwa uzalishaji wa makaa kwa kutumia vitagaa vyenye ukubwa wa kidole unaowania uzalishaji hadi katika ngazi ya kibiashara. |

## 1.2 Vigezo vinavyotumika kupima faida za mradi

| Vikundi | vipimo | Yaliyo afikiwa katika kipindi cha ukaguzi | Sehemu ya kumbukumbu ya ukaguzi. | Yatakayo afikiwa katika kipindi cha mradi. |
|---|---|---|---|---|
| Upunguzi na uondowaji wa hewa chafu. | makadirio ya hewa kaa iliyotoka katika eneo la mradi ukilinganisha kama mradi haungekuwepo. | 0 | | 0 |
| | makadirio ya hewa kaa iliyotoka katika eneo la mradi ukilinganisha kama mradi haungekuwepo. | 4,652,312 $tCO_2e$ | 3.2.4.5 | 10,218,962 $tCO_2e$ |
| Ukubwa wa msitu. | Kwa miradi ya REDD: Idadi ya hekta zilizopungua kupoteza misitu katika eneo la mradi uliopimwa dhidi ya mazingira yasiyo ya mradi | Takwimu hazipatikani - muundo wa mradi hauwezi kutoa hesabu ya hektari. | | Takwimu hazipatikani - muundo wa mradi hauwezi kutoa hesabu ya hektari. |
| | Kwa miradi ya ARR. Idadi ya hekta zilizoongezeka katika eneo la mradi uliopimwa dhidi ya mazingira yasiyo ya mradi | Hautumiki | | hautumiki |
| Uboresho wa usimamizi wa ardhi | Idadi ya hekta za ardhi ya misitu iliyopo ambayo mifumo ya IFM4 imetokea kama matokeo ya shughli za mradi huo | Haitumiki | | Haitumiki |

| Vikundi | vipimo | Yaliyo afikiwa katika kipindi cha ukaguzi | Sehemu ya kumbukumbu ya ukaguzi. | Yatakayo afikiwa katika kipindi cha mradi. |
|---|---|---|---|---|
| | ikilinganishwa tena na hali isiyo ya mradi. | | | |
| | Idadi ya hekta za ardhi isiyo ya misitu ambayo usimamizi wa ardhi umeboreshwa imefanyika kama matokeo ya mradi ikilinganishwa tena na hali isiyo ya mradi. | Haitumiki | | Haitumiki |
| Mafunzo | Idadi ya wanajamii walio ongeza ujuzi baada ya mafunzo kama sehemu ya mradi | 426 (ikihusisha vikundi vya mashule) wakitembelea miradi endelevu ya kilimo | 2.1.1. | >1,0000 |
| | Idadi ya wanajamii wakike waliongeza ujuzi baada ya mafunzo kama sehemu ya mradi | Kati ya 200 (Ikihusisha vikundi viwili vya wanawake ambao wameweza kuanzisha kilimo endelevu) | 2.1.1. | >500 |
| uajiri | Idadi ya watu walio ajiriwa ili kuendeleza mradi | 326 (ambao takriban 90% wametokea eneo la mradi na Kaunti ya Taita taveta) | 2.1.1., 4.3 | Makadirio ya mda mrefu ya uajiri kwa mradi wa KCRPI ukitazamia asilimia 90% ya watu wanaotoka katika eneo la mradi. |
| | Idadi ya wanawake walio ajiriwa ili ku endeleza mradi | 87 (takriban 27%) | 2.1.1. | Makadirio ya mda mrefu kati ya asilimia 20-30 ya waajiri |
| Hali za maisha. | Idadi ya watu ambao Maisha yao yaliboreka kutokana na mradi, na kuongezeka hali ya mapato yao. | Asilimia 33% ya wakaazi wa eneo la mradi walipokea faida za mradi kama vile kulipiwa karo ya watotot | 2.1.1. | Asilimia 33% ya wakaazi wa eneo la mradi walipokea faida za mradi kama vile kulipiwa karo ya watoto |

| Vikundi | vipimo | Yaliyo afikiwa katika kipindi cha ukaguzi | Sehemu ya kumbukumbu ya ukaguzi. | Yatakayo afikiwa katika kipindi cha mradi. |
|---|---|---|---|---|
| | | wao, ajira na miradi ya maji. | | wao,ajira na miradi ya maji. |
| | Idadi ya wanawake ambao Maisha yao yaliboreka kutokana na mradi kwa kuongezeka kwa hali yao ya mapato | Vikundi viwili vya wanawake walio jihusisha na ukulima endelevu katika ngazi za kibiashara | 2.1.1. | Vikundi viwili vya wanawake walio jihusisha na ukulima endelevu katika ngazi za kibiashara. |
| Afya | Idadi ya watu ambao huduma zao za afya zimeboreshwa kama matokeo ya mradi ikilinganishwa tena na hali isiyo ya mradi | Maabara ya voi≈36,000 wagonjwa kutoka 2015-2017 | 2.1.1. | Maabara ya voi: ≈46,000 – angalau wagonjwa 1000 kwa mwezi tangu ilipoanzishwa mwaka wa 2014 machi. |
| | Idadi ya wanawake ambao huduma zao za afya zimeboreshwa kama matokeo ya mradi ikilinganishwa na hali isiyo ya mradi. | Ikiangaziwa katika uhasibu wa kaunti, karibu ya asilimiahamsini wanaohitaji matibabu ni wanawake pamoja na wanachama wa GLOW. | 2.1.1. | Ikiangaziwa katika uhasibu wa kaunti karibu ya asilimia hamsini wanaohitaji matibabu ni wanawake pamoja na wanachama wa GLOW |
| Elimu | Idadi ya watu ambao wameweza kupata elimu bora imeongezeka ikilinganishwa na hali isiyo ya mradi | • Idadi ya waliolipiwa karo: 2,899<br>• Madarasa: 1 likiwa na wanafunzi 40<br>• Madawati: Kwa shule moja sawa na wanafuzi 40 | 2.1.1. | • Idadi ya waliolipiwa karo:2,899<br>• Madarasa:1 likiwa na wanafuzi 40<br>• Madawati: kwa shule moja sawa na Wanafunzi 40 |
| | Idadi ya wanawake ambao wameweza kupata elimu bora imeongezeka ikilinganishwa na hali isiyo ya mradi | Nusu ya waliolipiwa karo ni wasichana | 2.1.1. | Asilimia 47 ya waliolipiwa karo ni wasichana |

| Vikund i | vipimo | Yaliyo afikiwa katika kipindi cha ukaguzi | Sehemu ya kumbukumbu ya ukaguzi. | Yatakayo afikiwa katika kipindi cha mradi. |
|---|---|---|---|---|
| Maji | Idadi ya watu walioweza kupata maji safi kama sehemu ya mradi ikilinganishwa na hali isiyo ya mradi. | Kulingana na utafiti Takriban ya asilimia tatu (3%) ya miji imeweza kunufaika na miradi ya maji kutoka KCRP kama vile uchibaji wa visima na utegaji wa maji kutokana na miamba | 2.1.1. | Kulingana na utafiti Takriban ya asilimia tatu (3%) ya miji imeweza kunufaika na miradi ya maji kutoka KCRP kama vile uchibaji wa visima na utegaji wa maji kutokana na miamba |
| | Idadi ya wanawake walioweza kupata maji safi kama sehemu ya mradi ikilinganishwa na hali isiyo ya mradi | Ikiangaziwa katika uhasibu wa kaunti, takriban asilimia Hamsini (50%) ya wanajamii walioweza kupata huduma za maji safi ni wanawake na wasichana | 2.1.1. | Ikiangaziwa katika uhasibu wa kaunti, takriban asilimia Hamsini (50%) ya wanajamii walioweza kupata huduma za maji safi ni wanawake na wasichana |
| Mai sha | Idadi ya wanajamii ambao maisha yao yameboreshwa kama tukio la mradi | Mbali na kuboresha afya, elimu na maji, pia kuna kamati tatu kuu (LCC, kamati za masomo na mashirika ya jamii) ambayo yameimarishwa kupitia KCRP. Kupitia kamati hizi jamii imeweza kuibua hisia imara ya kujiamulia | 2.1.1, 4.1.2 | Mbali na kuboresha afya, elimu na maji, pia kuna kamati tatu kuu (LCC, kamati za masomo na mashirika ya jamii) ambayo yameimarishwa kupitia KCRP. Kupitia kamati hizi jamii imeweza kuibua hisia imara ya kujiamulia |
| | Idadi ya wanawake ambao maisha yao yameboreshwa kama tukio la mradi. | Angalau asilimia thelathini na tatu (33%) ya wanakamati ni wanawake | 2.1.1. | Angalau asilimia thelathini na tatu (33%) ya wanakamati ni wanawake |

| Vikundi | vipimo | Yaliyo afikiwa katika kipindi cha ukaguzi | Sehemu ya kumbukumbu ya ukaguzi. | Yatakayo afikiwa katika kipindi cha mradi. |
|---|---|---|---|---|
| Uhifadhi wa bionuwai | Mabadiliko katika idadi ya hekta kwa kiasi kikubwa imeboresha mradi kueza kuhifadhi bio-nuwai ikilinganishwa na tukio kabla ya mradi | 169,741.38 | 5 | 169,741.38 |
| | Idadi ya kimataifa iliyo hatarini au spishi walio hatarini wamenufaika kwa kupungua kwa vitisho vya kuangamizwa kama shughli za mradi ikilinganishwa na tukio kabla ya mradi | 4-pundamilia aina ya grevi (wakike), mbwa mwitu wa afrika (wakike) ,tai wa uso wa aina ya lappet na wale wa rangi nyeupe mgongoni | 5.1.2. | 4-pundamilia aina ya grevi (wakike), mbwa mwitu wa afrika (wakike) ,tai wa uso wa aina ya lappet na wale wa rangi nyeupe mgongoni |

## 1.3 Maelezo ya mradi

Mradi wa **Kasigau Corridor REDD+ Phase II – The Community Ranches** inakadiriwa kupunguza hewa kaa zaidi ya tani milioni 40 za $CO_2e$ ambazo zingekua zimeenda kwa anga kutokana na uharibifu wa misitu kwa miaka thelathini ya mradi. Mradi wa Kasigau Corridor REDD+ Phase II – the Community Ranches unapatikana kusini mashariki mwa Kenya, katika Kaunti ya Taita-Taveta, Mkoa wa Pwani. Ni takriban kilomita mia na hamsini (150) kaskazini magharibi mwa mji wa Mombasa. Eneo la mradi linahusisha ardhi yote ijulikanayo kama Taita Ranch, Mgeno Ranch, Maungu Ranch, Kasigau Ranch, Wangala Ranch, Kambanga Ranch, Dawida Ranch, Washumbu Ranch, Amaka Ranch, Sagalla Ranch, Ndara Ranch, Choke Ranch, Kutima Ranch, na Marungu Hills conservancy area, na jumla ya hektari 169,741.38 (ekari 419,440). Mradi ulianza 1-Januari 2010 na utakamilika tarehe 31-Desemba 2039. Muda huu wa ufatiliaji ($M_5$) ni wa tano na ulianza tarehe 1-januari -2015 na ukaisha Desemba 31- 2017. Hii ni stakabadhi ya muhtasari wa ripoti ya Project Implementation v 2 iliyotolewa tarehe 11/05/2018.

Mradi wa Kasigau Corridor REDD+ una lengo la kutoa misaada ya kifedha kutokana na soko la hewa kaa (carbon) ulimwenguni kwa kufanya yafuatayo:

- Kupunguza kiwango cha hewa chafu kwa kadri tani 40,000,000 kwa muda wa miaka thelathini (30) ambao ndo muda wa mradi, kwa kusaidia kuzuia uharibifu zaidi wa misitu kwa maeneo ya mradi na yale yanapakana na eneo la mradi.
- Kuongeza thamani ya kifedha kwa miradi iliyokua ikihifadhi misitu hapo awali, kuacha ukataji wa misitu kwa eneo la mradi na kuleta maendeleo endelevu katika jami zilizo maeneo ya mradi ili tuendelee kuhifadhi misitu na viumbe vilivyoko hata baada ya muda wa mradi.
- Kuhifadhi speshi za wanyama pori wanaotambulika kuwa katika hatari ya kuisha kama vile tembo wa Afrika (Loxidonta africana), Duma (Acinonyx jubatus), pundamilia (Equus grevyi), mbwa mwitu wa Afrika (Lycaon pictus), Simba (Panther leo) na aina zingine hamsini (50) za mamalia wakubwa wanaolidwa na askari pori kutoka Wildlife Works.

- kuhifadhi hactari elfu 169,741.38 ya misitu inayopatika katika mradi wa Kasigau corridor na kuweza kulinda bionwai pamoja na kuleta miradi endelevu kwa jamii inayopakana na sehemu zetu za mradi ili waweze kuona manufaa za kuhifadhi misitu.
- Kuwekeza mapato yanayotokana na mradi wa carbon na kuweza kuleta miradi endelevu katika jamii ili waweze kupunguza ukataji wa miti.
- kusaidia jamii kuhifadhi misitu na wanyama pori kupitia elimu itakayo wawezesha kutafuta njia mbadala kama vile kilimo endelevu.
- Kupanua mradi wetu wa kilimo endelevu na kuanzisha maeneo ya utunzi wa miche kwa jamii ili tuwe na njia mbadala za kilimo na kuni kuongezeka ili kuondoa haja ya wananchi kuanza kuvamia misitu jirani.
- Kutambua, kuelimisha na kuanzisha upanzi wa miti katika maeneo ya jamii ilituwe na mahali jamii wanaweza kupata kuni, hii itapunguza jamii kuvamia na kuharibu misitu.
- kutekeleza elimu kwa jamii kupitia vikundi vya akina mama, shule na zinginezo kama vile Marungu Hills Conservancy Association.
- Kuongezeka kwa bionuwai, utafiti na kujenga soko la miradi ya kitalii inayopatikana katika Kasigau Corridor.
- Kupanua ubunifu wa mradi wetu wa makaa zingira ili kupata njia mbadala ya kuni na yale makaa mengine yanayotoka kichakani ili kukidhi mahitaji ya matumizi ya kawi katika jamii inayopatikana katika mradi Kasigau Corridor REDD+.

Mradi wa Kasigau Corridor REDD+ Project awamu ya mbili umeafikia viwango vya juu kwa utoaji faida unaotokana na utunzi wa mazingira na pia kuweza kuangazia uhifadhi wa bionuwai.

**Manufaa yanayopatika na kuzuia mabadiliko ya tabia nchi**
Kuna ushahidi wa kutosha unaonyesha kuwa kuna mabadiliko ya tabia nchi katika maeneo ya mradi. Tangu jadi jamii zinazoishi kwa eneo la mradi wamekuwa wakitegemea sana kilimo. Eneo la mradi ni baadhi moja wapo ya maeneo ambayo hayana rotuba ya kufanya kilimo nchini Kenya.  Mvua imepungua kwa miaka kadha iliyopita, hii imesababisha kudorora kwa upanzi katikka mda unaostahili. Shida hii itaongezeka kutokana na mabadiliko ya hali ya anga kwa miaka kadha ijayo. Matokeo ya ukosefu wa mavuno yamesababisha wakulima kuendelea kufungua maeneo ya misitu kwa matarajio ya kupata mvua ya kutosha. Tunashirika uwengezeko wa uharibifu wa misitu kama hali za hewa zitazidi kudorora. Ukosefu wa mavuno unasababisha uwindaji haramu. Idadi ya wanyama pori asili wanaweza kujikimu wakati wa ukame, lakini pia hutaabika iwapo kuna mvua chache na joto jingi. Hii inamaanisha kwamba wanyama hawa wako katika hatari ya kuwindwa.

**Faida zinazotokana na kuifadhi bionuwai**

- Eneo la mradi Area ina aina ya pundamilia wa grevi ambao wako hatarini kwenye orodha ya IUCN Red. Eneo la Mradi inaweza kuwa na asilimia 3% ya idadi ya punda milia wa aina ya grevi ambao wanakisiwa kuwa 750 katika mwaka wa 2008.
- Eneo la mradi Area ni eneo wanapopatikana mbwa mwitu wa afrika (Lycaon pictus). Mbwa hawa wameweza kunaswa picha za camera zilizoko eneo la mradi ambao pia wako hatarini kulingana na orodha ya IUCN Red.
- Duma na simba ambao pia wako katika orodha za wanyama ambao wako katika hatari ya kuisha kulingana na IUCN Red wapo katika maeneo ya eneo la mradi. Inakisiwa idadi yao kuwa Zaidi ya 30 katika eneo la mradi.
- Eneo la mradi ni mojawapo ya kundi la Eastern Arc Mountain Global Hotspot kama inavyofafanuliwa na shirika conservation International. Ndani ya eneo la mradi Pamoja na nje ya mradi kuna aina nyengine za wanyama kama vile:
    - Taita Apalis
    - Taita Thrush

kupitia uhifadhi wa misitu inakadiriwa viwango vya hewa chafu vimeweza kupungua kutoa tani 10,218,962 hadi 4,256,903 t katika kipindi cha (1 Januari 2015 hadi 31 Disemba 2017). Upungufu huu umeweza kutokana na uhifadhi wa misitu katika eneo la mradi.

Eneo la mradi ni makao ya wanyama zaidi ya aina 50 ya mamalia wakubwa, aina zaidi ya 20 ya popo), ndege (zaidi ya speshi 300), pundamilia wa aina ya grevy (Equus grevyi), Duma (Acinonyx jubatus), Simba (Panthera leo) na zaidi ya Tembo 500 wa Afrika (Loxidonta africana) zilizo orodheshwa kuwa hatarini kwenye orodha ya IUCN Red. Mradi imeendelea kulinda na kuimarisha viumbe hai kupitia doria dhidi ya ujangili na Wanyamapori inayo fanywa na maaskari wa Wildlife Works na idara tofauti zinazo punguza migogoro dhidi ya binadamu na wanyama pori. Katika kipindi hiki cha ufuatiliaji wa mradi, maaskari wa Wildlife Works wanajivunia kuongezewa maaskari wengine Zaidi wakiwemo akina dada. Mwaka wa 2013 ulionyesha upungufu katika idadi ya matukio ya uwindaji haramu haswa tembo na hata makundi mengine.

Tangu mwanzo, mradi umetoa faida kubwa katika jamii. Hii ni pamoja na kuwaajiri wafanyikazi kwenye kiwanda cha ushonaji nguo, maaskari wa Wildlife Works, na kazi zinginezo tofauti. Mradi huu pia umetoa msaada kwa wanafunzi kwa kuwalipia karo ya shule na pia kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule zilizo kwenye eneo la mradi. Pia mradi umeanzisha mipango kadhaa kwa ajili ya ukuzaji na usambazaji wa miti ya matunda na aina ya miti asili kwa ajili ya kukuza misitu ya eneo hilo. Mradi umeongeza mipango kadhaa kwa ajili ya usambazaji ajira na kupunguza shinikizo juu ya rasilimali za eneo la mradi, kama vile kiwanda cha sabuni na kiwanda cha makaa zingira. Katika kipindi cha ufuatiliaji cha M5 (1 Januari 2015 - 31 Desemba 2017) Mradi umetoa faida kubwa katika jamii. Hii ni pamoja na kutoa ajira ya kudumu kwa watu zaidi ya 300 na wengine wa ziada kila siku. Mradi umetoa faida kubwa za kielimu katika jamii, ikiwa ni pamoja na karo kwa wanafunzi katika shule za sekondari na hata Chuo Kikuu ambacho kinafika kima cha shilingi 5,393,601 Katika kipindi hiki cha ufuatiliaji wa mradi. Zaidi ya shilingi milioni 14 zimetumika kwa miradi ya jamii zilizopendekezwa na jamii kupitia kamati zao. pia umetoa ufadhili katika miradi 5 ya maji kwenye jamii na kutoa zaidi ya miche 33,493 ya matunda na ya miti asili kwa ajili ya kupandwa katika maeneo ya jamii. Kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa watoto wa kike. Shirika la Wildlife Works limesaidia kutafutia vikundi vya wanawake na vya wanaoishi na ulemavu soko kwa bidhaa wanazo zitengeneza/kuunda. Katika kipindi cha ufatiliaji wa mradi vikundi hivi viliweza kupata shilingi milioni moja kutokana na mauzo.

USA Headquarters: 242 Redwood Highway, Mill Valley, CA 94941
T: 415.332.8081 | F: 415.332.8057 | www.wildlifeworks.com